

UFUGAJI WA NYUKI HUZUIA MIGOGORO BAINA YA BINADAMU NA WANYAMAPORI

Matumizi ya uzio wa mizinga ya nyuki


Utundikaji wa mizinga ya nyuki pembezoni mwa shamba huzuia tembo kufikia mazao lakini pia huongeza kipato kwa mkulima kutokana na mazao ya nyuki. Tembo huogopa nyuki kwa sababu nyuki huwadunga kwenye mkonga, macho na mdomo.

Mahitaji

- Mizinga ya nyuki
- Waya wa kuzungushia uzio na kushikia mizinga
- Vipande vya bati
- Majani ya kufunika juu ya mzinga kwa ajili ya kivuli
- Nguzo za miti yenye uwezo wa kuchipua



Jinsi ya kutundika mizinga ya uzio



Faida za kutumia uzio wa mizinga ya nyuki

- Kupata mazao ya nyuki ambayo huongeza kipato. Mazao hayo ni asali, nta, chavua, majana, gundi ya nyuki na sumu ya nyuki.
- Nyuki huchavusha mazao na hivyo kuongeza kipato na kuongeza usalama wa chakula.
- Matunda na mbegu zitokanazo na maua yaliyochavushwa na nyuki huwa ni vyenye vyenye ubora hivyo kuongeza uzalishaji.
- Nyuki husaidia uchavushaji wa mimea ya asilii na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu ambayo huchangia kwenye huduma mbalimbali za mfumo wa kiikolojia kama vile kupunguza hewa ukaa, mazao ya misitu, hewa safi na kuhifadhi vyanzo vya maji.

Kwa mawasiliano zaidi;
Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania
S.L.P. 661 Arusha, Tanzania
Simu: +255 27 254 9571
Barua pepe: barua@tawiri.or.tz



UFUGAJI BORA WA NYUKI KWA UTUNZAJI WA MAZINGIRA, UTATUZI WA MIGOGORO NA KUONGEZA KIPATO



Ufugaji wa nyuki husaidia kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato

FAIDA ZA UFUGAJI NYUKI

- Kujipatia mazao ya nyuki; asali, nta, majana, chavua, sumu ya nyuki, gundi ya nyuki
- Uchavushaji wa mimea
- Uhifadhi wa mazingira
- Uhifadhi wa bionuwai
- Kujipatia kipato
- Kupata fedha za kigeni
- Husaidia katika kupunguza migogoro baina ya wananchi na wanyamapori, hususani tembo
- Kupata dawa
- Kupata malighafi viwandani (asali, nta, gundi ya nyuki)
- Hutumika katika mila na desturi mbalimbali

Mahitaji ya nyuki katika mazingira

- Makazi
 - Chakula
 - Maji
 - Gundi
- Hakikisha eneo unalofugia nyuki lina mahitaji haya na pia lina **usalama** na **kivuli**

MIZINGA YA NYUKI

Mzinga ni makazi ya nyuki yaliyotengenezwa na binadamu

1. Mizinga ya jadi

Ipo ya aina mbalimbali kama vile magogo, vikapu, vyungu, vibuyu n.k. Masega ya mizinga hii hayahamishiki

2. Mizinga ya kisasa

Aina kuu mbili za mizinga ya kitanzania ambayo ni *Mzinga wa miche* na *Mzinga wa Vihunzi*. Masega ya mizinga hii yanahamishika.

Mzinga wa miche



Mzinga wavihunzi



Zana nyingine muhimu kwa ufugaji wa nyuki

Mavazi ya kinga yenye:

- Ovaroli
- Buti
- Utaji wa uso
- Mipira ya mikono



Vifaa vingine saidizi

Bomba la moshi



Brashi ya nyuki



Patasi ya mzinga